

Kifungu cha 8 Kufunguliwa kwa Orodha ya Kusubiri – Tangazo la Uuzaji na Ufikiaji

Idara ya Nyumba na Masuala ya Jamii ya Texas (TDHCA) inatangaza kufunguliwa kwa orodha ya kusubiri ya mpango wake wa Vocha ya Chaguo la Nyumba Jumatatu, Mei 2, 2022. Mpango huu hutoa fedha kupitia Idara ya Makazi na Maendeleo ya Miji ya Marekani ili kulipa sehemu ya kodi ya kila mwezi kwa familia zenye sifa katika mamlaka ya TDHCA.

TDHCA itakubali maombi ya awali ya mtandaoni ya orodha ya kusubiri kuanzia 8:00 a.m., Saa za Kati, Jumatatu, Mei 2, 2022, hadi 5:00 p.m., Saa za Kati, Jumatatu, Mei 16, 2022. Kati ya maombi yaliyopokelewa, TDHCA itatumia mfumo wa bahati nasibu kuchagua kwa nasibu waombaji 500 kwa ajili ya kuwekwa kwenye orodha ya kusubiri. Kila mtu ana nafasi sawa ya kuchaguliwa ikiwa atatuma maombi siku ya kwanza au siku ya mwisho. Namba ya bahati nasibu pia itaamua mahali pa mwombaji kwenye orodha ya kusubiri. Hakuna uchunguzi wa kustahiki kama sehemu ya mchakato wa kutuma maombi ya awali. Mpango wa vocha wa TDHCA unafanya kazi katika eneo la kaunti 34 pekee. Orodha ya eneo la kaunti 34 inaweza kupatikana katika tovuti ya <https://www.tdhca.state.tx.us/section-8/docs/ServiceAreas.pdf>.

Kuomba mtandaoni katika kipindi ambacho maombi yamefunguliwa, jaza maombi ya awali katika: <https://www.waitlistcheck.com/application/form.php?ID=3087-TX901>. Maombi yote lazima yapokewe kupitia zana ya maombi ya mtandaoni. Maombi yaliyotumwa kwa faksi, yaliyotumwa kwa mkono au ya barua pepe hayatapokelewa.

Watu wenye ulemavu ambao unawazuia kutuma maombi mtandaoni wanaweza kupiga simu 800-237-6500 ili kufanya mipango maalum ili wafanyakazi waweze kuwasaidia kukamilisha maombi kwa wakati ili wajumuishwe katika mchakato wa bahati nasibu. Maombi hayo yote lazima yafanywe kabla ya 5:00 p.m., Saa za Kati, Jumatatu, Mei 16, 2022.

Waswali yanaweza kuelekezwe kwenye namba 800-237-6500.

Waombaji ambao hawana mtandao wa intaneti wanaweza kuangalia katika rasilimali za karibu kama vile kompyuta kwenye maktaba iliyo karibu yao.

Waombaji lazima wachukuliwe kuwa wana mapato ya chini sana, yaani mapato yao ya kila mwaka lazima yawe 50% au chini ya mapato ya wastani ya eneo (AMI). Hata hivyo, 75% ya kaya ambazo TDHCA itazihudumia lazima ziwe na mapato ya chini sana yaani mapato yao ya mwaka lazima yawe 30% au chini ya AMI. Upeo wa juu kabisa wa mapato ya kaya kwa kila eneo la kaunti 34 zinazohudumiwa unaweza kupatikana katika <https://www.tdhca.state.tx.us/section-8/docs/S8-AMI-CountyChart.pdf>

Waombaji 500 watawekwa kwenye orodha ya kusubiri kwa bahati nasibu. Ikiwa hutapokea uthibitisho kutoka kwenye mfumo kwamba maombi yako yamewasilishwa kikamilifu, maombi yako hayatapewa namba ya bahati nasibu. Kuwekwa kwenye orodha ya kusubiri haimaanishi kwamba mwombaji anastahili kusaidiwa.

Taarifa zaidi inaweza kupatikana katika <https://www.tdhca.state.tx.us/section-8/announcements.htm>.